**Noa Bongo - Jenga Maisha Yako!**

**Utandawazi : Kukimbilia Mijini Kutelekeza Vijiji Nigeria**

**Autor : Sam Olukoya**
**Redaktion : Yann Durand**
**Übersetzung : Anne Thomas**

---

**3 Stimmen……………….Sauti 3**

- **Junger Sprecher 1 ………Msimuöizi wa kiume 1**
- **Junge Sprecherin 1………..Msimulizi wa kike 1**
- **Sprecher(in)………………..Msimulizi wa kike 2**
- **als Off-stimme (Reportage)**

---

**Für die O-Tone dazu : 2 Männer**

- **2 zwanzigjährige Männer**

---

**Vorspann LbE ……………………Kiashirio cha Kipindi**

**SEHEMU YA KWANZA – REPORTAGE : REPOTI**

**Sprecherin 1 : ….Msimulizi wa kike:** Habari gani ! Natumai nyote hamjambo!

**Msimulizi wa kiume 1 :** Leo katika mfulululizo wa vipindi vyetu maalum juu ya utandawazi tutazungumzia kuhusu miji ambayo inatanuka ….

**Msimulizi wa kike 1 :** …….ambayo inafurika wakati watu wakizidi kumiminika kutoka vijijini kwa ajili ya kutafuta kazi na maisha bora…..

**Msimulizi wa kiume 1 :** Kama matokeo miundombinu ilioko inazidi kuwa chini ya shinikizo zito.

**Msimulizi wa kike 1 :** Vitongoji duni na mitaa ya mabanda inazidi kuongezeka na hali ya maisha inazidi kuwa mbaya sana kila uchao.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Tunaelekea Lagos mji mkubwa kabisa nchini Nigeria ukiwa na idadi ya watu milioni 10 hadi milioni 13……

**Msimulizi wa kike 1 :** ………………ambapo hapo tutakutana na mkulima kijana ambaye amekuwa akitimiza matumaini yake.

**Msimulizi wa kiume 1 + Msimulizi wa kike 1 :**

Kwa hiyo fungeni mikanda yenu tayari kwa safari!

**………………….Manuscript……………….**

**1.Atmo: ville**

**Msimulizi wa kike 2 :** Akeem Gbenro ana umri wa miaka 20.Kupenda kwake miji mikubwa kumemfanya aachane na maisha yake akiwa kama mkulima.Kwa hiyo ameondoka kwenye kijiji chake na kwenda Lagos ilioko umbali wa kilomita 300.Vijana wengi huwa wanavutiwa na Ndoto ya Lagos.Wana hakika kwamba maisha bora yanawasubiri mjini humo.

**2.O-Ton**

Nimekuja Lagos kutafuta kazi.Nimeondoka kwenye kijiji changu kwa sababu kulikuwa na okosefu mkubwa wa ajira. Nilikuwa mkulima wa muhogo katika kijiji hicho.Hakuna fedha zinazopatikana kwenye ukulima.Mmojawapo wa marafiki zangu alikuja Lagos na kuwa tajiri sana kwa hiyo na mimi nataka kufanya kama alivyofanya yeye na ndio sababu niko hapa.

**3. Atmo : Stadt**

**Msimulizi wa kike 2 :** Akeem Gbenro katu hakuwahi kwenda shule na kitu pekee alichojifunza ni kulima.Kwa hiyo wakati alipowasili mjini alifanya yake  yale kama wanavyofanya vijana wengi wanaokuwa katika hali kama yake.

**4.O-Ton :** Tokea nilipowasili Lagos nimekuwa muendesha pikipiki mjuzi na hii ni pikipiki yangu.

**5.Atmo : Motorrad startet**

**Msimulizi wa kike 2 :** Haikuchukuwa muda mrefu kwa Akeem Gbenro kuanza kukosa raha.

**6.O-Ton**

Nimekuwa nikijipatia fedha kwa kuwa dereva wa pikipiki lakini nilikuwa nikitaraji kuwa ningelipata fedha nyingi zaidi mjini Lagos.Nimekata tamaa kwani sivyo nilivyotegemea.

**7.Atmo Verkehr + O-Ton +Atmo Verkehr wieder hoch………..**

Kila siku nimekuwa nikiona ajali.Ni hatari kuendesha pikipiki hapa Lagos.Ningelikuwa bado niko kijijini nisingediriki kujihatarisha kwa ajili ya kujipatia kipato.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Kabla ya Lagos Akeem hawakuwahi kukanyaga mji wowote ule mkubwa.Wakati mara ya kwanza alipowasili mjini humo alipata fadhaa.

**8. O-Ton**

Kuna uhalifu mwingi mjini Lagos.Hakukuwa na uhalifu wowote ule kijijini.Uhalifu uliopo hapa unanitisha na pia kuna matatizo mengine mengi.Huko kijijini hakuna polisi wanaowakamata watu na kuwapaleka kituoni bila ya sababu.Lakini hapa **nimenyanyaswa na**

polisi mara kadhaa. Jambo ambalo halikuwahi kunitokea katu nilipokuwa kijijini.

**9.Atmo : Gesang auf dem Markt ……..**

**Msimulizi wa kike 2 :**

Katika kijiji mkulima huyo alikuwa hahitaji kwenda kufanya manunuzi. Lakini kwa kuwa mkaazi wa mjini inabidi ende sokoni.

**10.O-Ton**

Ninakuja sokoni kununuwa samaki,nyama na maharage. Bei za vyakula ni ghali zaidi mjini Lagos wakati maisha kijijini sio ya ghali mno.

**Msimulizi wa kike 2 :** Wakati wa jioni Akeem hurudi Makoko mtaa wa mabanda ulioko kwenye kiunga cha Lagos.Karibu nyumba zote zilioko juu nguzo zinaonekana kuelea juu ya wangwa.

**11. Atmo :Wasser**

**Msimulizi wa kiume :** Ni furaha ilioje kurudi nyumbani kwa mashua!

**Msimulizi wa kike :** Lakini kumbuka kwamba hilo sio eneo la makaazi na ingelikuwa wanaweza watu wangeliondoka kwenye mitaa ya mabanda.

**12.O-Ton**

Watu hapa huishi kwenye maji kwa sababu nyumba zake zinakuiwa sio ghali sana.Lakini hazina faraja kutokana na kutokuwa na maji na umeme na kwa sababu zimejengwa kwa kutumia tabaka la mbao zilizogandishwa pamoja.

**13.Atmo Landstraße (Archiv)**

**Msimulizi wa kike 2 :**

Mowe ni mji mdogo uliopo kati ya Lagos na Ibadan.Hapo ndipo anapoishi Solomon Israel na ndugu zake watatu wa kiume.Wote wanaishi kwenye chumba kimoja kidogo pembezoni mwa barabara kuu inayokatiza vijiji.

**14.O-Ton**

Tumeamuwa kukaa hapa Mowe ambapo tumejipatia mahala pa kujistiri.Hatuna ndugu yoyote yule huko Lagos.Nimepata kazi hapa ambapo baada ya kazi huwa ninaweza kurudi nyumbani na kupumzika.Lakini huko Lagos sina nyumba na ingelibidi nitafute kazi na hata kama ningeliweza kupata kazi suali ningeliishi wapi ?Hilo ndio tatizo la huko inabidi uwe na mahala pa kuishi ili kuweza kufanya kazi.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Solomon anawajuwa watu wengi wenye umri wa miaka ya ishirini kama yeye ambao hawakuwa na matarajio makubwa ya kupata kazi.Wengine hutumbukia kwenye dimbwi la uhalifu na kuja kuwa wahanga wa mawasiliano yasiopendeza.Lakini Solomon yuko furahani na maisha yake nje ya mji.

**15. O-Ton**

Maisha hapa yametulia na ya heshima . Tuko furahani na hatuna dhiki yoyote ile.Kuna upendo hapa.  Kitu pekee ninachohitaji hapa ni amani,uhuru wangu na utulivu wa akili yangu.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Akeem Gbenro katu asingekubali kubadilisha maisha yake na yale ya Solomon kwa yeye hakuna kinachoweza kulinganishwa na maisha ya kijamii katika miji mikubwa.

**16.O-Ton**

Maisha mjini Lagos ni mazuri kwa sababu ya jinsi vile watu wanavyofikiri jinsi wanavyovaa na kujimwaga barabarani.

**Msimulizi wa kike 2 :**

**………au kukutana kwenye vilabu vya pombe.**

**17.Atmo bar …………..kilabu cha pombe ….**

**18.O-Ton**

Na hapa ndipo ninapokuja kupumzika baada ya kazi. Huwa nakuja na marafiki zangu na kujipatia vinywaji kidogo. Nimezoweya kuja kuburudika hapa wakati wa usiku lakini kijijini hakuna mahala kama hapa.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Suala vijana kukimbilia mijini kutoka vijijini limeusha wasi wasi kwa serikali ya Nigeria.Inasema miundo mbinu ya mjini imekuwa chini ya shinikizo kubwa sana.Lakini tatizo kubwa zaidi ni kwamba kilimo kimekuwa kikidharauliwa kwa sababu vijana kama Akeem Gberon wanayatelekeza mashamba yao.

**MWISHO WA SEHEMU YA KWANZA**

---

**SEHEMU YA PILI**

**Msimulizi wa kiume 1 na Msimulizi wa kike 1 tu……**

**Msimulizi wa kiume :** Je Lagos ina mitaa ya mabanda mikubwa kabisa duniani ?

**Msimulizi wa kike :** Hapana, Nairobi nchini Kenya ndio kuna kitongoji duni kikubwa kabisa duniani ambapo watu milioni moja nukta nne wanaishi kwenye mitaa ya mabanda , hiyo ikiwa ni asilimia 60 ya idadi ya watu wa mji huo.

**Msimulizi wa kiume :**

**Kwa hiyo kuna mitaa ya mabanda duniani kote ?**

**Msimulizi wa kike :** Ndio katika kila bara lakini hususan katika nchi zinazoendelea. Umoja wa Mataifa unasema kuna watu zaidi ya bilioni moja wanaoishi kwenye mitaa ya mabanda na vitongoji duni. Iwapo hakuna kitakachobadilika kukabiliana na hali hiyo idadi hiyo itafikia watu bilioni mbili katika kipindi cha miaka 30 ijayo.

**Msimulizi wa kiume :** Lakini kwa nini takwimu hiyo inaongezeka licha ya watu kutambuwa matatizo yake ?

**Msimulizi wa kike :** Kwa muhtasari kuna sababu kuu tatu ..kwamba kiwango cha vifo kinashuka chini kwa hiyo kuna watu wengi zaidi duniani. Halafu kuna watu kama vile Akeem ambao huondoka vijijini. Na hatimae utandawazi ambao Umoja wa Mataifa unasema unaiwezesha nchi ya kimaskini kuendelea bali pia unatanua pengo kati ya matajiri na maskini.

**Msimulizi wa kiume :** Ni nini kinachoweza kufanywa kuboresha hali ya maisha katika mitaa ya mabanda?Ili kwamba wakaazi wake waweze kuwa na maji,umeme,barabara na usafi wa mitaro na maji taka?

**Msimulizi wa kike :** Naam tatizo ni kwamba mitaa hii ya mabanda mikubwa kabisa  haiko rasmi.Watu wanaoihi hapo hawazimiliki nyumba zao wala kuzikodisha na majengo yenyewe kwa kawaida yamejengwa kinyume na sheria.

**Msimulizi wa kiume :** Kwa hiyo hakuna msaada kwa watu hao ?

**Msimulizi wa kike :** Sio rahisi.Hata hivyo viongozi wa dunia wamejizatiti kutowa ahadi ya kuboresha hali ya maisha kwa angalau wakaazi milioni 100 wa vitongoji duni kabla ya mwaka 2020.

**Abspann ………………Funga Kipindi**

**Msimulizi wa kike :** Na hapo ndio tumefikia tamati ya Noa Bongo - Jenga Maisha Yako!Asante kwa kusikiliza kipindi hiki juu ya utandawazi kilicholenga kurupuko la watu kuvikimbia vijiji na taathira ya kufurika mijini.Ni kipindi cha Deutsche Welle kilichotayarishwa na Sam Olukoya na Yann Durand. Ili kujuwa zaidi au ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki tafadhali nenda kwenye tovuti yetu www.dw-world.de/lbe: Usikose kujiunga nasi wakati mwengine! Kwaheri !